



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. HWT/L1/7/86

18.04.2023

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Tarime kupitia kibali cha kutekeleza ikama na bajeti kwa ajira mpya katika mwaka wa fedha 2022/2023 chenye **Kumb.Na.FA.97/228/01 TEMP /06** cha tarehe **6.April.2023** kilichotolewa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Anatangaza nafasi za kazi kwa wananchi wa Tanzania wenye sifa na ujuzi wa kujaza nafasi zifuatazo

MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III NAFASI (12)

1.1 MAJUKUMU YA KAZI

- i. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao,kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa Mipango ya maendeleo ya kijiji.
- iv. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- v. Kutafsiri na kusimamia sera,sheria na taratibu.
- vi. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa,umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- vii. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya kitaalamu katika kijiji.
- viii. Kusimamia,kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji.

1.2 SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Awe Mtanzania.
- ii. Awe na Elimu ya Kidato cha Nne au cha Sita.
- iii. Awe amehitimu mafunzo ya Astashahada (cheti) katika moja ya fani za Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii na Sayansi ya sanaa kutoka chuo cha Serikali za Mitaa cha Hombolo –Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.
- iv. Awe na umri wa **miaka 18** au zaidi na asiwe na *umri unaozidi miaka 45*.
- v. Awe na afya njema, mchapa kazi na mwenye utayari wa kufanya kazi mahali popote katika vijiji vya Halmashauri ya Wilaya ya Tarime.

2 NAMNA YA KUOMBA

- a. Maombi yote ya ambatishwe na nakala za vyeti vya taaluma, mafunzo, vyeti vya kuzaliwa, pia na kitambulisho cha NIDA vilivyothibitishwa na mahakama au na mtu yeyote aliyeidhinishwa na Serikali.
 - b. Testimonials' 'Provisional Results', Statement of Results; Hati za matokeo ya kidato cha nne na sita **HAVITAMBULIKI**
 - c. Waombaji wote waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe kuwa vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika ya **TCU** na **NECTA**
- 3 Watumishi wote waliowahi kufanya kazi katika Utumishi wa Umma wakaacha, wakastaafu, wakastaafishwa au wakafukuzwa hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- 4 Vyeti vyote vitafanyiwa uhakiki kwa kushirikiana na mamlaka husika za **NECTA**, **TCU** na Vyuoaombaji walivyosomea na endapo itagundulika mwombaji amehusisha vyeti vya kughushi kwenye maombi yake atachukuliwa hatua za kisheria.
- 5 Mshahara utalipwa kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Serikali **TGS 'B'**


6. MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI

Maombi yatapokelewa katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Nyamwaga, mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **09.05.2023** saa **9:30** alasiri.

Tunawakaribisha wote wenye sifa zilizotajwa hapo juu kuwasilisha maombi yao kwa utaratibu ulioelekezwa. Maombi yote yatumwe kupitia anwani ya:-

**Mkurugenzi Mtendaji (W),
S. L. P 16,
TARIME.**

Tangazo hili lkinapatikana kwenye mbao za matangazo za Halmashauri ya Wilaya ya Tarime pamoja na kwenye tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Tarime ambayo ni: www.tarimedc.go.tz.



Solomon I. Shati

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
TARIME.**

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME**